# KISWAHILI KARATASI YA KWANZA

# ANSWERS

# KCSE 2010

Coordinated by KENPRO, Macjo Arcade, 4th Floor, Suite 15E, Off Magadi Road, Ongata Rongai
|Tel: +254202319748 | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com/

## Kiswahili Karatasi ya 1

1. **Mtahiniwa azingatie muundo wa insha ya wasifu.**
Mtahiniwa anahitajika kuandika mambo muhimu yanayohusiana na elimu. Ahakikishe kuwa yanayowasilishwa ni mambo chanya. Mfano wa hoja:
- Mwaka wa kuzaliwa na alikozaliwa mhusika.
- Wazazi wake ni akina nani.
- Juhudi za wazazi au wafadhili kumwelimisha.
- Alikosomea na juhudi zake katika elimu.
- Vikwazo/changamoto alizoweza kukabiliana nazo katika elimu yake.
- Ufanisi wake katika elimu ya juu katika Chuo Kikuu.

2. **Mtahiniwa aeleze maana ya ufisadi.**
Hii ni insha ya maelezo. Mtahiniwa azue hoja na kuzitetea.
Hoja:
- Serikali kubuni asisi tekelezi ya kitaifa ya kampeni dhidi ya ufisadi ambayo huchunguza na kutoa mapendekezo dhidi ya ufisadi.
- Wafisadi kuchukuliwa hatua. Wengi wamefikishwa mahakamani huku maafisa wa umma wanaohusishwa na ufisadi wakifutwa kazi na kisha kufikishwa mahakamani.
- Kuimarisha taasisi za uongozi, haki, sheria na utangamano kupitia kwa mpango wa ufadhili wa GJLOS ambao umejumuisha makundi ya kijamii.
- Kuanzisha halmashauri ya kitaifa ya kutoa ushauri kwa tume ya kupambana na ufisadi ambayo imejumuisha makundi ya kidini, vyama vya wataalamu, sekta ya kibinafsi na ile ya wafanyakazi.
- Tume za Kisheria za kuchunguza kashfa za ufisadi kutumiwa mara kwa mara inapohitajika mathalan Tume ya Samwel Bosire kuchunguza kashfa ya Goldenberg, ile ya Hotel ya Grand Regency n.k.
- Kuanzishwa kwa ofisi ya mchunguzi maalum wa kusikiliza malalamiko ya umma ambapo umma unaweza kuripoti kuhusu ufisadi.
- Nafasi pana kutolewa kwa wanahabari na umma kuripoti kuhusu ufisidi.
- Elimu ya uraia.
- Kampeni zilizofadhiliwa na serikali zote zikiwa dhidi ya ufisadi – kupitia kwa vyombo vya habari, mabango, vipeperushi.
- Sera ya serikali inayohitaji kila idara au asasi iunde kamati ya kupambana na ufisadi.
- Watumishi wa umma kuhitajika kutangaza utajiri wao.
- Kuhitaji watu wote nchini kutangaza ushuru waliolipa kila mwaka.

3. **Hii ni insha ya mjadala**
Mtahiniwa azue hoja za kuunga na pia kupinga kauli iliyotolewa. Kisha aonyeshe msimamo wake.

**Hoja za Kupinga.**
- Lugha zetu za kienyeji ni kielelezo cha utamaduni wetu. Umoja wa kitaifa hauwezi ukapatikana katika mazingira ambayo taifa linatukuza utamaduni wa kigeni.
- Lugha zetu za kwanza ambazo ndizo lugha za kienyeji hutuwezesha kuwa na ukakamavu wa kujieleza, kuwa wabunifu wa kuingiliana na watu wengine kwa wepesi kuliko wale wanaosema lugha ambazo si za awali.
- Hazina ya maadili, ujuzi na hekima ya jamii imo katika utamaduni wao. Utamaduni huu hauwezi ukatenganishwa na lugha. Hivyo kudai kuwa hatupaswi kusema kwa lugha zetu za kwanza ina maana kuwa hazina yote ya maadili yetu pamoja na hekima ya kiasili vitapotea.
- Lugha zetu asilia huwa na msingi bora wa kujifunzia lugha nyingine. Utafiti umedhihirisha kuwa wasemaji bora wa lugha za kigeni ni wale mahiri katika lugha zao asilia.

- Utafiti umedhihirisha kuwa kikwazo kikuu cha umoja wa kitaifa ni mitazamo hasi ambayo inaendelezwa na baadhi ya watu ambao wanaogopa kuweko kwa umoja huu wala si lugha za kienyeji.

**Hoja za kuunga mkono**

- Watu wanapoendelea kushikilia lugha zao za kwanza ina maana kuwa hawaachi desturi na tamaduni zao. Twajua kuna migongano na tofauti kubwa kati ya tamaduni tofauti. Katika hali hii inakuwa vigumu kupata utamaduni mmoja unaoweza kuwa ugwe wa kuwaunganisha Wakenya.
- Lugha zetu asilia husheheni mitazamo hasi kuhusu majirani wetu ambao hawatumii lugha moja nasi. Kutupilia mbali lugha hizi na kuchukua lugha moja kama Kiswahili kutatuweshesha kutohoa hisia hasi kwa wenzetu. Katika hali hii, pana uwezekano mkubwa wa kuwa na umoja wa kitaifa.
- Hivi sasa tuna ndoa za asili mbalimbali za lugha. Iwapo tutadai kila mwanandoa aendeleze lugha yake katika ndoa ile tutawakanganya watoto wetu. Wataibukia kukosa mielekeo mizuri.

**Msimamo**

Ili kuleta umoja wa kitaifa tunahitaji kuchota yaliyo bora kutoka kwa tamaduni zetu na kujenga utamaduni unaoweza kukubalika na kila Mkenya. Kisha tuteue lugha moja ya Kiafrika kama Kiswahili na kuifanya lugha ya maingiliano kati ya Wakenya wote.

**4. Hii ni methali**

Mtahiniwa aandike kisa kimoja tu kuthibitisha ukweli kwamba lolote mtu alifanyalo watu hawakosi kusema. Kwa hivyo mtu asijali mradi kile anachofanya ni halali.